


# Sekta binafsi inahitaji sera, mfumo thabiti wenye udhibiti uliokamilifu

**Ubadilishaji holela na ghafla wa sera unaonekana kuumiza viwanda. Jambo hilo limeathiri pia kilimo cha korosho ambayo uchunguzi unaonyesha pamoja na kudhibitiwa ili kulipa kodi, bado haifanyi vizuri.**

Veneranda Sumila

Sekta binafsi nchini inataka kuwapo na mazingira thabiti yanayoeleweka ya kisera na udhibiti yatakaowezesha wawekezaji, watekelezaji na wateja kuwa katika hali ya kufanya maamuzi ya muda mrefu wakiwa na uhakika.

Uthabiti katika masuala ya kisera pamoja na udhibiti kwa muda mrefu kumefanya kuwapo na walakini katika uendeshaji wa sekta ya biashara.

Jambo hilo litasaidia mazingira yanayoweza kuleta mabadiliko ya soko na teknolojia yanayotokea mazingira ya ufanyaji biashara.

Pia, ni dhahiri kuwapo kwa utulivu katika sera, kutachochea shughuli ambazo hazijasajiliwa, kusajiliwa. Kauli hii imetolewa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Shirikisho la wenye Viwanda Tanzania (CTI) aliyestaafu, Christine Kilindu.

Mtendaji huyu mstaafu anaamini kwamba kutotabirika kwa udhibiti na mabadiliko ya mara kwa mara ya sera, kumefanya sekta ya viwanda kusuasua, huku viwanda vingi vikishindwa kuleta ushindani.

"Serikali imekuwa ikibadili sera kila mara bila kuwapo na mazungumzo ya kutosha na sekta binafsi. Hali hiyo imeiletea matatizo makubwa sekta ya viwanda," alisema Kilindu.

Wakati viwanda vikipata tozo mbalimbali, jambo hili linachangia ukuaji mdogo wa viwanda, kwani tozo hizo huwa hazisaidii kiwanda kuingia katika soko la ushindani.

"Wenye viwanda wanalazimika kila mara tozo zinapotokea, wajadili gharama mpya za uzalishaji, Pia hulazimika kuangalia gharama mpya za utangazaji wa mabadiliko ya bei na gharama nyingine. Serikali lazima ibadilike na kuhakikisha kwamba kunakuwapo na mabadiliko yenye kueleweka na yenye tija ya kisera," alisema Kilindu.

Mazingira yasiyoeleweka ya kisera yanayochochewa na mabadiliko holela wakati mwingine husababishwa na kuwapo na mamlaka nyingi za udhibiti zinazotoza viwango tofauti za tozo wakiwa na masharti tofauti ambayo wakati mwingine yanagongana au kubatilishana kutoka mamlaka moja hadi nyingine.

"Taasisi nyingi hutumia muda mwingi kwenda kwenye mamlaka moja hadi nyingine ikilipa tozo mbalimbali zilizo nyingi na zenye gharama kubwa."

"Tunaiomba Serikali kuwa na eneo moja au taasisi moja ambayo itapewa tozo za mamlaka zote husika. Taasisi hiyo ndiyo ihusike kugawa kwa mamlaka husika," alisema Kilindu.

Kwa maoni yake taasisi hiyo moja ndiyo itakayokusanya tozo na kodi za mamlaka mbalimbali na kuziwasilisha zinakohusika.

Kuwapo kwa mamlaka nyingi za udhibiti kumeongeza gharama kwa viwanda kiasi cha kuvifanya visiwe na ushindani na bidhaa zinazotoka nje ambazo udhibiti wake ni mdogo.

"Hatusemi kwamba bidhaa zisiingizwe lakini tunataka uwapo ushindani wa haki. Serikali inatakiwa kuhakikisha kwamba waigizaji wa bidhaa mbalimbali wanalipa kodi zinazotakiwa na kusiwepo na upenyo wa kukwepa ulipaji wa kodi. Kwa upande mwingine viwanda nchini visilazimishwe kulipa kodi zisizokuwa za lazima," alisema Bi Kilindu.

Anaamini kwamba kwa kutokuwepo na hali ya kutabirika katika masuala ya udhibiti na ubadilishaji holela wa sera, ni kikwazo kikubwa kwa uendelezaji wa biashara zinazotambulika. Alisema kwamba kutokana na mazingira hayo watu wengi huamua kuendesha shughuli zao bila kuzisajili.

> **SAUTI ZA WANANCHI**
>
> **MEDISON KUBOJA, Dar es Salaam**
>
> **Nchi zote zilizoendelea Serikali za nchi zao ziliwekeza katika viwanda na pia kwenye usafiri wa reli. Serikal yetu ya Tanzania haina budi kuwekeza katika sekta hiyo kwa dhati na kuandaa sera nzuri ya uchumi jumuishi.**
>
> **JOHANNES SIONG'O, Dar es Salaam**
>
> **Ni muhimu sana kuanzisha nguvu kazi yenye maadili ambayo itaweza kurahisisha ufanyaji wa biashara nchini Tanzania, wafanyakazi wengi wa serikali hawako tayari kwa ajili ya soko huria, wana hisia kali juu ya haki zao, juu ya udhibiti wa kila kitu badala ya kutoa huduma / kuwezesha (maadili ya kazi yenye kuleta tija yanahitaji kupewa kipaumbele ili kuendana na kasi ya mabadiliko ya dunia ya sasa)**

### Udhibiti sekta ya korosho

Kwa mujibu wa taarifa ya kisera iliyotolewa na Jukwaa Lisilo la Kiserikali la Kilimo (ANSAF), sekta ya korosho ndiyo inadhibitiwa kuliko sekta nyingine duniani, huku ikiingiza pato kubwa la kodi kupitia mauzo yake.

Pamoja na ukweli huo sekta hiyo haipati faida.

"Imebaki kuwa mzalishaji wa korosho zinazoenda kubanguliwa bara la Asia," imesema sehemu ya taarifa ya ANSAF.

Changamoto zinazokumba sekta hii siku zote zimekuwa zikimuumiza mkulima, lakini yote hayo yamo ndani ya muundo wa mfumo wa udhibiti kwenye sekta ya korosho.

Hali ilivyo, taarifa ilisema kwamba, Serikali imetaka kuendeleza zao hilo la korosho lakini taasisi zilizokabidhiwa jukumu hilo mara nyingi zimekuwa haziangalii mahitaji ya soko.

Walichokuwa wakifanya muda wote ni kusikiliza sauti za wanasiasa na kushughulika nazo.

Kitu kinachotakiwa kwa sasa kufanywa kwa manufaa ya taifa na kwa wakulima, ni kwa nchi kuhakikisha kwamba zao la korosho linafanyiwa kazi nyumbani kwa asilimia 100. Ili kufanikisha hilo taifa linahitaji kuwa na sera ya kuaminika isiyobadilika kiholela na na mamlaka za udhibiti ambazo zipo wazi na zinazoendana na mahitaji ya soko na si mahitaji ya wanasiasa.

### Sekta ya utalii

Shirikisho la Taasisi za Utalii nchini (TCT) limebaini kwamba, kitendo cha kubadilisha sera bila kuangalia kiundani nini kitatokea kabla ya kuanza kwa utekelezaji, huathiri sekta ya utalii na wadau wanaojihusisha na utalii pamoja na usafiri.

Inaeleweka kwamba bajeti ya utalii huenda kwa mzunguko wa mwaka ikiwamo ya uwekaji wa nafasi ya malazi na usafiri. Kitendo cha kubadilisha mambo katikati ya mwaka mara nyingi husababisha watalii kusitisha safari zao.

"Ubadilishaji wa ghafla wa mambo bila tahadhari huvuruga bei ya bidhaa na mahitaji mengine na inawezekana pia eneo hilo likaelezwa na mawakala kama eneo ambalo haliaminiki," anasema Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCT, Richard Rugimbana.

Anasema kuwa, kwa sasa taasisi yake inaunga mkono namna ambavyo Serikali inawasikiliza kuhusu maoni wanayotoa.

Taarifa ya kidunia ya ushindani ya mwaka 2014 katika sekta ya utalii imesema kuwa, moja ya vikwazo vikubwa vya uendelezaji wa sekta ya utalii Tanzania ni kutokueleweka kwa sera.

Pia, kodi kubwa, mfumuko wa bei na sarafu kutokuwa imara.

### Shauri la kujifunza

Kabla ya bajeti ya mwaka 2014/2015 Serikali na wadau sekta binafsi walikubaliana ongezeko la ushuru la asilimia 10 kwa bidhaa za bia. Wakati bajeti inasomwa ushuru ukaongezeka kwa asilimia 20. Kwa Kiwanda cha Bia cha Tanzania Breweries Limited, moja ya walipaji wakubwa wa kodi, ongezeko hilo lilikuwa na maana ya kusimamisha uwekezaji, kupunguza wafanyakazi.

Hivyo kutokana na kupungua kwa mahitaji na hii itasababisha pia kupungua kwa kiwango cha ulipaji kodi.

***Kwa mrejesho tutumie ujumbe mfupi wa maneno kupitia 0786240172. Tufanye nini tuboreshe mazingira ya biashara? Washiriki wawili, watapewa muda wa maongezi wa Sh30,000.***

UKURASA HUU UMEDHAMINIWA NA
BEST-Dialogue
Doing business, let's make it easy - and fair
Kufanya biashara kwa haki - bila vikwazo